JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI-TAMISEMI

KUMB.Na KSS/FV/2017/02 Shule ya Sekondari **Kiteto**

Namba za simu S.L.P 86, Kibaya.

Mkuu wa shule: 0682 498556 Tarehe: ……

Makamu mkuu wa shule: 0714 181113

Matron: 0786 309117

Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi …….

……..

S.L.P ……

……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KITETO HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO MKOA WA MANYARA MWAKA 2017.

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2017 tahasusi ya **CBG**. Shule ya Sekondari Kiteto ipo umbali wa Kilometa 2 Mashariki mwa mji wa Kibaya. Usafiri wa pikipiki/taksi unapatikana kutoka stendi ya mabasi Kibaya kwa Shilingi 2,000/= mpaka 3,000/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **17/7/2017**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti tarehe **16/7/2017.**Mwisho wa kuripoti ni tarehe **30/7/2017.**

Mambo muhimu ya kuzingatia

1. **Sare ya shule**
   a) Sare ya shule hii ni sketi ya kijivu (grey). Mshono ni marinda nane kama inavyoonekana hapo chini.

      Muhimu: urefu wa sketi ipite magoti, isiwe ya kubana na iwe ya kitambaa kizito. Kwa wanafunzi wakiislamu ivuke vifundo vya miguu.

   b) Shati mbili au zaidi nyeupe za mikono mirefu.
   c) Tai ndefu ya kijivu yenye miraba mshazari ya rangi nyeupe.
   d) Sweta la kijivu.
   e) Rangi ya hijabu (juba) ni nyeupe (kwa wanafunzi wa kiislamu).
   f) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi.
   g) Nguo za kushindia (shamba dress): sketi nyeusi mbili mshono wa boksi na fulana (shingo ya duara) mbili au zaidi za rangi ya blue zisizo na maandishi yeyote.
   h) Sare za michezo shuleni:Track suit ya bluu bahari na raba nyeupe.

      N.B: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA SHULENI NA NGUO NYINGINE TOFAUTI NA ZILIZO AGIZWA.

2. **Ada na michango yas hule**
   a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/=. Unaweza kulipa shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule iitwayo **KITETO SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT** namba **5011100015** katika benki ya **NMB** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).
   b) Michango mingine.
   (i) Shilingi 15,000/=kwaajili ya ukarabati wa samani.
   (ii) Shilingi 6,000/=kwaajili ya kitambulisho na picha.
   (iii) Shilingi 20,000/=kwaajili ya taaluma.
   (iv) Shilingi 30,000/=kwaajili ya kuwalipa wapishi,Walinzi na vibarua wengine.
   (v) Shilingi 2,000/=kwajili ya nembo ya shule.

(vi) Shilingi 10,000/= kwajili ya huduma ya kwanza. Muhimu: Unashauriwa mwanao ajiunge na mfuko wa Bima ya Afya (CHF) hapa Kiteto kwa gharama ya 10,000/= kama hajajiunga na Bima nyingine.
(vii) Shilingi 20,000/= kwaajili ya mtihani wa kujipima (MOCK)
(viii) Shilingi 10,000/= kwaajili ya kukodisha godoro kwa muhula.
(ix) Shilingi 5,000/= kwaajili ya tahadhari. (haitarejeshwa)

Jumla ya ada na michango yote kwa mwanafunzi ni 188,000/=

c) Mahitaji muhimu kwa mwanafunzi.
Mwanafunzi ana takiwa kuja na vitu vifuatavyo:
(i) Rimu moja ya karatasi (kwa mwaka)
(ii) Vitabu vyote vya tahasusi anayosoma (CBG) kwaajili ya matumizi yake binafsi.
(iii) Dissecting kit.
(iv) Scientific calculator.
(v) Mashuka mawili au zaidi rangi ya bluu bahari, blanket imoja, foronya mbili na mto, chandarua kimoja rangi nyeupe.
(vi) Vyombo vya chakula (sahani ya udongo, bakuli la udongo, kijiko na kikombe)
(vii) Ndoo kubwa moja na ndogo moja.
(viii) Kwanja moja, jembe moja, reki moja, mifagio miwili (ya ukili)
(ix) Sanduku la bati (trunker moja)

MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi.
(ii) Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au namtu yeyoteyule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usio kubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo waususi uliokubalika na uongozi wa shule.
(vii) Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(viii) Uvutaji wa sigara.
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayo vunja sheria za nchi.
(xii) Kutembelea nyumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xiv) Kudharau Bendera yaTaifa
(xv) Kufanya jambo lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Muhimu: Siku ya kutembelea wanafunzi ni jumamosi ya mwisho wa mwezi kuanzia saa 4:00-7:30 mchana tu ili kuepuka usumbufu usio wa lazima labda kama imelekezwa vinginevyo Aidha mwanafunzi asipewe mchango wowote wa shule bila barua kutoka kwa mkuu wa shule.

Viambatisho naFomu Muhimu

a) Fomuya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga wa Hospitali ya Serikali.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARIKITETO!

KIMARO J.

MKUU WA SHULE.

KITETO DISTRICT COUNCIL

KITETO SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

From: Kiteto Secondary School,
P. O. Box 86,
Kibaya – Kiteto.
Date: ……

Medical Officer,
……..
P. O. Box …….
……

Full Name: ……...
Please examine the above named student to her fitness for entrance to this school in form five year 2017.

- Blood current ……..……..
- Stool …….
- Urinal analysis …….
- T.B test ……
- Syphilis…….
- Ears……
- Chest ……
- Spleen ……..
- Eyes test……
- Abdomen test……

(**Check course of pregnancy**)

Additional information e.g. physical defects or permanent infection such as family chronic diseases etc..
……..
.....
.....
…….

MEDICAL CERTIFICATE
(**To be completed by medical officer**).
I have examine the above named and considered that she is fit/unfit for enrolment to the school above.
Name …… Signature ……. Date…….
Station …… Designation …….

Official Stamp

NB: At the time of examination please treat the individual for an illness you note.